Jina: ______________________________ Tarehe: ______________

Nambari ya mwanafunzi(**KNEC ASSESSMENT NO.**) ______________________

Gredi ____________________ Jinsia: Mvulana [ ] Msichana [ ]

Jina la shule ______________ Nambari ya Shule [ ][ ][ ][ ]

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha k[illegible] ya mwanafunzi**

**Viwango vya kutathmini**

| **ZOEZI** | **Kuzidisha matarajio 4** | **Kufikia matarajio 3** | **Kukaribia matarajio 2** | **Mbali na matarajio 1** |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kwa sauti **10** | Ana uwezo wa kusoma kwa kasi bila kusita. Anazingatia alama zote za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma bila kusita. Anazingatia baadhi ya alama za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma, isipokuwa anasitasita. Hazingatii alama za uakifisho. | Hana uwezo wa kusoma maneno mengi. Hazingatii alama za uakifisho. |
| Kusikiliza na kuzungumza **(alama 5)** | 5 | 4 | 2 - 3 | 0 - 1 |
| Sarufi/Ufahamu/ kuandika **(alama 35)** | 35 | 30 - 34 | 14 - 29 | 0 - 13 |

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## SEHEMU A:

1. **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

**Nitakuuliza maswali kisha utayajibu kwa Kiswahili.**

**a)** Ukimkosea mtu, utamwambiaje? **(Mwanafunzi ajibu)**
**b)** Ukitaka kuingia darasani, utasemaje? **(Mwanafunzi ajibu)**
**c)** Ukimuaga mgeni, utamwambiaje? **(Mwanafunzi ajibu)**
**d)** Ukiomba ruhusa ya kwenda kujisaidia, utasemaje? **(Mwanafunzi ajibu)**
**e)** Ukipewa zawadi, unapaswa kusema aje? **(Mwanafunzi ajibu)**

## KUSOMA KWA SAUTI

**Soma kifungu hiki kwa sauti.**

Mwili wangu ni zawadi muhimu inayoniwezesha kufanya mambo mbalimbali kila siku. Mikono yangu hunisaidia kushika vitu na kufanya kazi za mikono kwa ufanisi. Miguu yangu huniruhusu kutembea na kukimbia, ikinipa uhuru wa kuzunguka. Moyo wangu hupiga kwa nguvu, ukiniweka hai.

## SEHEMU YA B:
## UFAHAMU

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.**



Paliondokea mwanafunzi mtiifu. Jina lake ni Maria. Maria alipendwa na wazazi. Majirani pia walimpenda Maria. Shuleni walimu pia walimpenda. Maria alipendwa kwa utiifu. Hakukaidi mambo ya wakubwa wake. Mwisho wa muhula ulipowadia, Maria alituzwa zawadi. Alikuwa mwanafunzi mtiifu zaidi. Wanafunzi walimshangilia. Maria alifurahi sana.

**(a)** Ni nani aliyekuwa mtiifu? ______________________________

**(b)** Taja watu waliompenda mwanafunzi mtiifu.

______________________, ______________________

**(c)** Hakukaidi mambo ya ______________ wake. **(wakubwa, marafiki)**

**(d)** Mwanafunzi alituzwa wakati gani? ______________________
**(Mwanzo wa muhula, Mwisho wa muhula)**



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## SARUFI

**Tumia jedwali hili kuunda majina ya vifaa vya darasani**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| da | ba | ru | bu | a |
| u | ta | wa | nge | fu |
| ki | ch | o | la | ti |

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

4. ______________________________

**Andika sentensi hizi kwa wingi.**

5. Mimi ninasoma. ______________________________

6. Mimi ninacheza. ______________________________

7. Mimi ninaimba. ______________________________

8. Mimi ninalima. ______________________________

**Andika maneno haya vizuri.**

9. ikjiok - ______________________

10. emza - ______________________

11. apmri - ______________________

12. amte - ______________________




Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Andika kwa herufi ndogo**

13. DAWATI - ____________

14. SHEREHE - ____________



15. Huyu mnyama anaitwaje? ____________

16. Huyu mnyama ako na pembe ngapi? ____________

**Andika kinyume cha maneno haya**

17. Keti - ____________

18. Lala - ____________

19. Cheka - ____________

20. Kimbia - ____________

**(Tembea, Lia, Amka, Simama)**

**Andika nambari hizi kwa maneno.**

21. 9 - ____________

22. 7 - ____________

23. 4 - ____________

**Jaza pengo kwa kutumia 'Huyu au 'Hawa'**

24. ____________ wanasoma vizuri.

25. ____________ anacheza mpira.

## KUANDIKA

**Andika sentensi tano ambazo mwalimu atatamka.**

26. ____________

27. ____________

28. ____________

29. ____________

30. ____________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com